ISASP IOWA STATEWIDE ASSESSMENT of STUDENT PROGRESS

The University of Iowa
ITP Iowa Testing Programs

Kwa Familia,

Kurasa zifuatazo zinakuonyesha jinsi ya kufasiri Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi, ambayo inatoa muhtasari wa matokeo ya mwanafunzi katika mitihani ya hivi majuzi zaidi ya mpango wa Utathmini wa Maendeleo ya Wanafunzi katika Jimbo Lote la Iowa (ISASP). Mpango wa ISASP umekusudiwa kutoa maelezo kwa shule na familia kuhusu jinsi wanafunzi wanavyoendelea kulingana na Viwango Vikuu vya Elimu vya jimbo la Iowa.

Ukurasa wa 1 wa ripoti unaonyesha muhtasari wa matokeo ya mwanafunzi wako kwenye mtihani wa kila somo la mpango wa ISASP. Kuna alama ya kipimo ya mtihani wa somo, picha ya matokeo ya alama ya kipimo na kiwango cha mafanikio kulingana na alama ya kipimo. Maelezo kuhusu matokeo ya mwanafunzi wako yanatoa taarifa zaidi kuhusu maarifa na ujuzi wa wanafunzi wa kawaida katika kiwango cha mafanikio cha mwanafunzi wako.

Ukurasa wa 2 wa ripoti unaonyesha matokeo ya mwanafunzi wako katika Vitengo Vikuu vya Elimu vya jimbo la Iowa vinavyohusishwa na mtihani la kila somo. Vitengo ni sehemu mahususi za maudhui za kuangaziwa katika somo. Vitengo vimeorodheshwa kwa kila somo na pia asilimia ya maswali ambayo mwanafunzi wako alifaulu kujibu kwa kila kitengo imewekwa.

Ukurasa wa 3 unaonyesha matokeo ya mwanafunzi wako kwenye jaribio la sasa la mpango wa ISASP ikilinganishwa na alama ambazo mwanafunzi wako alipata miaka ya awali. Grafu hii inathibitisha mazungumzo kuhusu maendeleo ya mwanafunzi wako jinsi inavyoonyeshwa kwenye mabadiliko ya alama baada ya muda.

Ukurasa wa 4 unaonyesha matokeo ya mwanafunzi wako kwenye mtihani wa Kuandika. Alama ambazo mwanafunzi alipata katika sehemu nne (Uandishi wa Vidokezo, Ubunifu, Mpangilio na Matumizi ya Lugha) zimeonyeshwa, pamoja na alama za wastani za wilaya ya shule yako. Pia, matokeo ya mtihani yameonyeshwa kwenye utaratibu wa Kina cha Maarifa (DOK). Kila kipengele cha mtihani kimehusishwa na DOK inayoonyesha aina na kiwango cha kufikiria na kupambanua mambo ambacho mwanafunzi anahitaji. Sehemu inayoonyesha alama ambazo mwanafunzi wako alipata kati ya alama za jumla zinazoweza kupatikana katika kila kiwango cha DOK imeonyeshwa.

Unapokagua matokeo ya ISASP, chukua muda wa kuzungumza kuhusu matokeo pamoja na mwanafunzi wako. Uliza maswali na upate majibu kutoka kwa mwanafunzi wako kuhusu sehemu anazozielewa vizuri zaidi, usaidizi wa ziada anaohitaji na mambo ambayo humfurahisha mwanafunzi wako darasani. Wasilisha majibu haya na matokeo ya mtihani wa mpango wa ISASP kwa shule ya mwanafunzi wako ili ipate maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kukuza maendeleo ya mwanafunzi wako.

Wako mwaminifu, Mipango ya Mitihani ya Jimbo la Iowa

# ISASP — IOWA STATEWIDE ASSESSMENT of STUDENT PROGRESS

ISASP ni mpango mpya wa utathmini wa jimbo lote unaolingana na Viwango Vikuu vya Elimu vya jimbo la Iowa. Unatoa matokeo dhahiri na sahihi ya utathmini wa masomo ya mwanafunzi ambayo yanafaa na yanaweza kuchukuliwa hatua na wanafunzi, wazazi, walimu na jimbo. Mwongozo huu unafafanua jinsi ya kusoma **Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi**.

## *Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi*

## *Ukurasa wa 1 kati ya 4*

ISASP
IOWA STATEWIDE ASSESSMENT of STUDENT PROGRESS

RIPOTI YA MWANAFUNZI

JINA ... WANZA JINA LA MWISHO-ELAMATHSCI
KITAMBULISHO CHA JIMBO#0123456789
JINA LA SHULE (5678)
JINA LA WILAYA (1234)

**1**

MAJIRA YA KUCHIPUA YA 2019 — DARASA LA 5

Jimbo la Iowa limejitolea kutoa tathmini ya ubora wa hali ya juu kwa wanafunzi wake. Mpango wa Utathmini wa Maendeleo ya Wanafunzi Katika Jimbo Lote la Iowa (ISAPS) umeainishwa kulingana na Viwango Vikuu vya Elimu vya Jimbo la Iowa.

Matokeo haya yatawapa walimu, wazazi na wanafunzi maelezo muhimu kuhusu matokeo ya mwanafunzi ambayo yanaweza kutumika kuelekeza masomo ili kusaidia kila mwanafunzi kwa njia bora zaidi.

**Muhtasari kuhusu matokeo ya JINA LA KWANZA katika ISASP**

| JUMLA YA SANAA ZA LUGHA YA KIINGEREZA | Alama ya Kipimo: **475** | Kiwango cha Mafanikio: **STADI** |
|---|---|---|

**2**



KIWANGO CHA JUU (999-999)
STADI (999-999)
BADO SI STADI (999-999)

Jumla ya alama ya kipimo ya Sanaa ya Lugha ya Kiingereza (ELA) ni mchanganyiko wa alama zako za kipimo za Kusoma (999) na Lugha/Kuandika (999).

Mwanafunzi katika kiwango hiki ana maarifa, ujuzi na uwezo wa kuwa stadi katika ELA. Hii inaweza kujumuisha uwezo wa kusoma, kuelewa na kuchambua maandishi ya fasihi na maelezo. Hii inaweza pia kujumuisha uwezo wa kuandika vipande madhubuti ambavyo vinafaa, vyenye mpangilio na vinavyotumia Kiingereza cha kawaida. Ukurasa wa pili wa ripoti hii unatoa maelezo kuhusu matokeo ya mwanafunzi wako katika nyanja za ELA.

Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu alama ya Jumla ya Sanaa ya Lugha ya Kiingereza ya mwanafunzi wako katika http://iowa.pearsonaccessnext.com/.

| HISABATI | ...ma ya Kipimo: **410** | Kiwango cha Mafanikio: **BADO SI STADI** |
|---|---|---|

**3**



KIWANGO CHA JUU (999-999)
STADI (999-999)
BADO SI STADI (999-999)

Mwanafunzi aliye katika kiwango hiki hajaonyesha maarifa, ujuzi na uwezo wa kuwa stadi katika somo la Hisabati. Ukurasa wa pili wa ripoti hii unatoa maelezo kuhusu matokeo ya mwanafunzi wako katika nyanja za somo la Hisabati.

Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu alama ya somo la Hisabati ya mwanafunzi wako katika http://iowa.pearsonaccessnext.com/.

| SAYANSI | Alama ya Kipimo: **551** | Kiwango cha Mafanikio: **KIWANG...** |
|---|---|---|

**4**



KIWANGO CHA JUU (999-999)
STADI (999-999)
BADO SI STADI (999-999)

**5**

Mwanafunzi ...ka kiwango hiki ana maarifa, ujuzi na uwezo wa kuwa st...di katika Say...ni pamoja na kutumia Desturi za Sayansi na Uhandisi na ...ana Zinazot...yanja Zote za Sayansi na kuonyesha na kuelewa kwa kina sayans... ...azingira, dunia na anga. Mwanafunzi anawasilisha maoni na dhana za ...a kutumia desturi changamani za sayansi. Ukurasa wa pili wa ripoti hii unatoa m...zo kuhusu matokeo ya mwanafunzi wako katika nyanja za Sayansi.

Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu alama ya somo la Sayansi ya mwanafunzi wako katika http://iowa.pearsonaccessnext.com/.

http://iowa.pearsonaccessnext.com/

Ukurasa wa 1 kati ya 4 — 000000-12345678-0000000

* Kumbuka: Ikiwa huoni alama **za mtihani ulioorodheshwa**, tafadhali wasiliana na shule ya mwanafunzi wako kwa maelezo zaidi. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu mpango wa ISASP na Ripoti ya Mwanafunzi Mahususi katika **http://iowa.pearsonaccessnext.com/**

### **1.** MAELEZO YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi, Kitambulisho cha Mwanafunzi cha Jimbo la Iowa, shule, wilaya na darasa huonyeshwa katika sehemu ya juu ya ukurasa wa kwanza.

### **2.** KIPIMO CHA MATOKEO

Kipimo cha Matokeo hutoa picha ya Kiwango cha Mafanikio ya mwanafunzi. Viwango vya alama kwa kila kiwango cha mafanikio huonyeshwa chini ya picha.

### **3.** ALAMA YA KIPIMO

Alama ya Kipimo ni alama ambayo inaruhusu ulinganishaji wa maendeleo katika madarasa na miaka yote.

### **4.** KIWANGO CHA MAFANIKIO

Kiwango cha Mafanikio huonyesha matokeo ya mwanafunzi kwenye mtihani na hutoa maelezo ya jumla ya kile ambacho mwanafunzi anafahamu na anaweza kufanya.

### **5.** MAELEZO YA MATOKEO

Maelezo ya Matokeo ni ufafanuzi wa jinsi ambavyo mwanafunzi anaelewa maudhui mahususi kwa kiwango cha darasa lake.

# ISASP — IOWA STATEWIDE ASSESSMENT of STUDENT PROGRESS

## *Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi*

## *Ukurasa wa 2 kati ya 4*

ISASP
MAJIRA YA KUCHIPUA YA 2019 | DARASA LA 5 | JINA LA KWANZA JINA LA MWISHO-ELAMATHSCI
KITAMBULISHO CHA JIMBO# 0123456789

ALAMA KATIKA NYANJA

Alama katika nyanja zinaweza kutoa maarifa kuhusu uwezo wa mwanafunzi wako na fursa za kujiimarisha. Katika majedwali yaliyo chini ya alama katika nyanja za mwanafunzi wako zinaonyeshwa kama asilimia sahihi katika kila aina.

| Alama za Uwanja wa K[illegible]OMA-ELA | Asilimia ya Ambayo Mwanafunzi Alifaulu |
|---|---|
| Mawazo na Maelezo Muhimu | 82% |
| Usanifu na Muundo | 60% |
| Ujumuishaji wa Maarifa na Maw[illegible] | 57% |

6

| ELA-Alama za Uwanja wa LUGHA/KUANDIKA | Asilimia ya Ambayo Mwanafunzi Alifaulu |
|---|---|
| Utafiti wa Kukuza na Kuwasilisha Maarifa | 37% |
| Uzalishaji na Usambazaji wa Uandishi | 83% |
| Aina na Mandhumuni ya Maandishi | 36% |
| Kanuni za Kiingereza cha Kawaida / Maarifa ya Lugha | 88% |
| Ufahamu na Matumizi ya Msamiati | 42% |

| Alama za Uwanja wa HISABATI | Asilimia ya Ambayo Mwanafunzi Alifaulu |
|---|---|
| Hesabu na Maarifa ya Aljebra | 40% |
| Nambari na Hesabu za Msingi wa Kumi | 60% |
| Nambari na Hesabu – Visehemu | [illegible]0% |
| Vipimo na Data | 48% |
| Jiometri | 57% |

7

| Alama ya Uwanja wa SAYANSI | Asilimia ya Ambayo Mwanafunzi Alifaulu |
|---|---|
| Sayansi za Maisha | 84% |
| Sayansi za Halisi | 92% |
| Sayansi za Dunia na Anga | 80% |

http://iowa.pearsonaccessnext.com/
Ukurasa wa 2 kati ya 4

### 6. VITENGO VIKUU VYA MASOMO VYA JIMBO LA IOWA

Vitengo Vikuu vya Masomo vya Jimbo la Iowa ni sehemu za maudhui na darasa za kuangaziwa ambazo hujaribiwa. Kwa mfano, *Mawazo na Maelezo Muhimu* ni kitengo cha Kusoma katika darasa la 5.

### 7. ASILIMIA YA ALIYOFAULU

Asilimia ya Aliyofaulu hutoa asilimia ya maswali ambayo mwanafunzi alijibu kwa usahihi katika kila Kitengo Kikuu cha Masomo cha jimbo la Iowa.

Mpango wa ISASP hutathmini:

- **Kusoma**
Kwa Madarasa ya 3 - 11
- **Lugha na Kuandika**
Kwa Madarasa ya 3 - 11
- **Hisabati**
Kwa Madarasa ya 3 - 11
- **Sayansi**
Kwa Madarasa ya 5, 8 na 10

# Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi


## Ukurasa wa 3 kati ya 4

ISASP
MAJIRA YA KUCHIPUA YA 2021 | DARASA LA 6 | JINA LA KWANZA JINA LA MWISHO-ELAMATHSCI
KITAMBULISHO CHA JIMBO#0123456789


### MAENDELEO

Maendeleo hubainishwa kwa kulinganisha alama ya sasa ya kipimo ya mwanafunzi na alama ya kipimo ya mwaka uliotangulia. Grafu ya pau iliyo hapo chini inaonyesha alama mbalimbali za kipimo zinazohusiana na kila kiwango cha mafanikio kwa madarasa ambayo yalifanya jaribio la ISASP. Alama za kipimo za mwanafunzi wako zimeonyeshwa kwenye grafu ya pau inayolingana kwa alama ya ✶ (nyota).

SANAA ZA LUGHA YA KIINGEREZA




HISABATI




VIWANGO VYA MAFANIKIO: BADO SI STADI | STADI | STADI ZAIDI

http://iowa.pearsonaccessnext.com/

Ukurasa wa 3 kati ya 4

## 8. MAENDELEO

Ukurasa wa Maendeleo hutoa maelezo kuhusu alama ya sasa ya mwanafunzi na alama zozote zinazohusishwa na mitihani ya awali ya mpango wa ISASP.

Pau zilizo na rangi zinazonyesha viwango vitatu vya mafanikio na alama za kipimo za mwanafunzi wako kwenye grafu ya pau kwa kutumia alama ya * (nyota).

Alama za kipimo kwa kila sehemu ya somo zimewekwa kwenye kipimo kimoja na zinaweza kulinganishwa moja kwa moja ili kubaini jinsi ambavyo matokeo ya mwanafunzi yamebadilika baada ya muda.


# Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi

## Ukurasa wa 4 kati ya 4

ISASP | | JINA LA KWANZA JINA LA MWISHO-ELAMATH
MAJIRA YA KUCHIPUA YA 2021 | DARASA LA 6 | KITAMBULISHO CHA JIMBO#0123456789

### ALAMA ZA JARIBIO LA KUANDIKA

Insha ya mwanafunzi wako ilipewa alama kulingana na vipengele vinne vya kuandika: Uandishi kutokana na Vidokezo, Ubunifu, Mpangilio na Matumizi ya Lugha. Unaweza kupata mtandaoni maelezo mahususi ya kila pointi ya alama inahusishwa na kila kipengele (http://iowa.pearsonasccess.com/rubrics/). Grafu hii inaonyesha alama ambazo mwanafunzi wako alipata kwa kila kipengele. Alama ya ✚ (ongeza) inaonyesha Alama ya Wastani ya Wilaya ya kila kipengele.




### KINA CHA MAARIFA (DOK)

Kila kipengee cha jaribio la ISASP kimebainishwa na kiwango cha kina cha maarifa (DOK). DOK au uwezo wa kufahamu mambo, unaonyesha aina na kiwango kufikiria na kupambanua mambo ambacho mwanafunzi anahitaji anapotumia kitu fulani. Jedwali linaonyesha sehemu inayoonyesha pointi ambazo mwanafunzi wako alipata kati ya jumla ya pointi zinazoweza kupatikana katika kiwango hicho cha DOK.

**10** Pointi Ambazo Mwanafunzi Alipata / Jumla ya Pointi Zinazoweza Kupatikana

| | ELA- KUSOMA | ELA - LUGHA/ KUANDIKA | HISABATI |
|---|---|---|---|
| Ujuzi, Tabia na Maarifa Yanayohitajika (DOK 1) | 7 / 10 | 6 / 12 | 6 / 18 |
| Kuelewa Dhana (DOK 2) | 10 / 17 | 7 / 13 | 5 / 11 |
| Upambanuzi wa Kina (DOK 3) | 4 / 7 | 3 / 8 | 3 / 10 |

http://iowa.pearsonaccessnext.com/

Ukurasa wa 4 kati ya 4

## 9. UTARATIBU WA KUANDIKA

Insha za mwanafunzi hupewa alama kulingana na vipengele vinne tofauti vya uandishi:
--Uandishi wa Vidokezo
--Ubunifu
--Mpangilio
--Matumizi ya Lugha
Grafu inaonyesha alama ambazo mwanafunzi wako alipata kwa kila kipengele. Alama ya + (kuongeza) inaonyesha Alama ya Wastani ya wilaya kwa kila kipengele.

Alama za mwanafunzi wako na ulinganisho wake na alama za wastani za wilaya, zinaweza kuonyesha sehemu ambazo anazielewa vizuri zaidi na zile ambazo anahitaji kuziboresha.

## 10. KINA CHA MAARIFA

Kina cha Maarifa (DOK) kinaonyesha aina na kiwango cha kufikiria na kupambanua mambo ambacho mwanafunzi anahitaji ili kujibu swali la mtihani. (DOK 3 inaonyesha kiwango cha juu cha uwezo wa kufikiria na kupambanua kuliko DOK 1). Jedwali linaonyesha sehemu zinazonyesha alama ambazo mwanafunzi wako alipata kati ya alama za jumla zinazoweza kupatikana katika kiwango hicho cha DOK.

Mpango wa ISASP huwapa maelezo wanafunzi, wazazi, waalimu na jimbo kuhusu jinsi wanafunzi katika jimbo la Iowa wanavyoendelea kulingana na Viwango Vikuu vya Elimu vya Jimbo la Iowa. Unakusudiwa kutoa maelezo muhimu kuhusu sehemu ambazo wanafunzi wanaendelea vizuri na sehemu ambazo wanaweza kuhitaji usaidizi wa ziada. Wanafunzi na wazazi wanahimizwa kukagua matokeo kwenye Ripoti ya Mwanafunzi Mahusus na kuwasiliana na shule zao ili wapate maoni ya ziada.